

**GRADE 4 MID TERM 3 DECEMBER 2021  
KISWAHILI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**I. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

***Mwalimu asome hadithi hii mwanafunzi akisikiliza kisha amwulize maswali.***

**KIHOTO, SHULE YANGU**

Kihoto ni shule nzuri. Ina madarasa makubwa na walimu wazuri. Ina bustani la maua ya kupendeza. Ina kiwanja kikubwa cha kuchezea. Ina maktaba yenye vitabu vya hadithi tamu. Ina ua ambao umeizunguka ili kulinda usalama wa wanafunzi. Shule hii huwa namba moja katika michezo.

- a) Taja shule inayozungumziwa katika hadithi. ***(Mwanafunzi ajibu)***
- b) Taja vitu mbalimbali vinavyopatikana katika shule hii. ***(Mwanafunzi ajibu)***
- c) Ni nini inapatikana kwenye maktaba ya shule hii? ***(Mwanafunzi ajibu)***
- d) Shule hii imezingirwa na nini? ***(Mwanafunzi ajibu)***
- e) Shule hii inaongoza katika nini? ***(Mwanafunzi ajibu)***

## II. KUSOMA KWA SAUTI.

***Soma hadithi ifuatayo kwa sauti mwalimu akisikiliza.*** (alama 10)

Bi Naliaka ni chifu wa kata ya Jipemoyo. Kata ya Jipemoyo iko katika kaunti ya Barakazi. Bi Naliaka anapenda kazi yake. Yeye huifanya kwa bidii na kwa unyenyekevu. Wakazi wa kata ya Jipemoyo wanampenda sana. Wao pia ni wachapakazi. Wanamheshimu chifu wao, Bi Naliaka sana.

Bi Naliaka huandaa mikutano ya kata yake kila Ijumaa katika ofisi yake. Wakazi wa Jipemoyo huhudhuria bila kulazimishwa. Chifu Naliaka huwafahamisha na kuwafunza mambo mengi akitumia video na rununu yake.

## III. SARUFI.

(Alama 20)

### 1. Andika kinyume cha vitenzi vifuatavyo.

(alama 5)

- a) anika - \_\_\_\_\_
- b) panga - \_\_\_\_\_
- c) simama - \_\_\_\_\_
- d) cheka - \_\_\_\_\_
- e) tandika - \_\_\_\_\_

2. **Andika sentensi zifuatazo kwa wingi.** (alama 3)

- a) Kipepeo yule anapendeza. \_\_\_\_\_
- b) Daktari anatibu mgonjwa. \_\_\_\_\_
- c) Mwalimu yule ni mrefu sana. \_\_\_\_\_

3. **Tegua vitendawili hivi.** (alama 4)

- a) Natembea na paa mgongoni. \_\_\_\_\_
- b) Kuku wangu hutagia miibani. \_\_\_\_\_
- c) Nyumba yangu haina mlango. \_\_\_\_\_
- d) Fimbo ya babu ina mafundo. \_\_\_\_\_

4. **Jaza pengo ukitumia sehemu zifuatazo za tarakilishi.** (alama 4)

**kiwambo, kipanya, kiibodi, kitufe**

- a) Daudi alibofya \_\_\_\_\_ na kufungua tarakilishi yake.
- b) Nilipiga chapa kwa \_\_\_\_\_ na maneno yakaonekana kwenye \_\_\_\_\_ cha tarakilishi.
- c) Mwalimu alitumia \_\_\_\_\_ ili kurudisha nyuma kielekezi cha tarakilishi kwenye kiwambo.

5. **Tumia viunganishi vifuatavyo kuunda sentensi.** (alama 4)

- a) kwa sababu \_\_\_\_\_
- b) pia \_\_\_\_\_
- c) na \_\_\_\_\_
- d) lakini \_\_\_\_\_

**IV. UFAHAMU.**

**(alama 10)**

**Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Hapo zamani walikuwapo ndugu watatu. Walipendana kama chanda na pete. Majina ya ndugu hawa ni Jitumoto, Jitumaji na Jituupepo. Jitumoto aliwasaidia ndugu zake kwa kazi ya kupika. Jitumaji alikuwa na kazi ya kuosha kila kitu na kufua nguo. Kila kitu kilikuwa safi kwa bidii ya Jitumaji.

Jituupepo alikuwa na kazi muhimu mno. Kila mtu alipata hewa ya kuvuta kwa sababu ya Jituupepo. Alipopumua alimpulizia kila mtu hewa ambayo inaleta uhai maishani.

a) Andika majina ya ndugu watatu waliotajwa. **(alama 2)**

---

b) Ni nani aliyewasaidia ndugu zake kwa kazi ya kupika? **(alama 2)**

---

c) Ni nani aliwasaidia wengine na uhai? **(alama 2)**

---

d) Jitumaji aliwasaidia ndugu zake kwa kufanya nini? **(alama 2)**

---

e) Unafikiri ni nani aliyefanya kazi nzuri na kwa sababu gani? **(alama 2)**

---